## Maswali

1. Kitu gani kiovu chenye Waisraeli walifanya baada ya kifo cha Yoshua?
2. Adui wa Waisraeli walikuwa nani?
3. Nani alikuwa nahodha wa Wakanaani?
4. Waisraeli waliuliza nani awasaidie na awasamehe?
5. Mungu alituma nani awasaidie washinde Wakanaani?
6. Baraka alienda kuona nani?
7. Debora alisema nani atapata utukufu kwa kushinda Sisera?
8. Mungu alisaidia Waisraeli namna gani kushida vita?
9. Nani aliuwa Sisera? Aliuwawa namna gani?
10. Waisraeli waliabudu nani kwa miaka arobaini?Walikuwa na amani?

## Majibu

1. Waisraeli walianza kuabudu sanamu.
2. Wakanaani walikuwa adui wa Waisraeli.
3. Sisera alikuwa nahodha wa Wakanaani.
4. Waisraeli waliuliza Mungu awasamehe na awasaidie.
5. Mungu alituma Baraka aongoze Waisraeli wapigane na Wakanaani.
6. Baraka alienda kuona Debora.
7. Debora alisema mwanamke atapata utukufu kwa sababu Baraka hakuamini Mungu kabisa.
8. Mungu alituma dhoruba kubwa. Farasi na magari zilikwama kwa matope. Wakanaani walitoroka.
9. Yaeli aliuwa Sisera. Aligonga msumari wa hema kwa kichwa chake.
10. Waisraeli waliabudu Mungu. Walikuwa na amani kwa miaka arobaini.

# SHULE YA JUMAPILI YA CBM

## Awamu ya 2    Mwaka wa 1

# 31 Debora na Baraka

**Kwa Biblia** Waamuzi mlango wa 4

### Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu husaidia watu wake wakiwa na imani

### Somo

Yoshua aliishi na akawa mtu mzee. Alikuwa kiongozi mzuri kwa watu. Yoshua aliongoza Waisraeli kwenda mpaka nchi ya Kanaani. Mungu alisaidia Waisraeli kupigana na kuchukuwa hiyo nchi. Mungu alipea kila kabila mahali pao pakuiishi. Kila jamii ilikuwa na kipande chao cha nchi. Waisraeli walikaa kwa nchi yenye Mungu aliwaahidi.

Baada ya kifo cha Yoshua Waisraeli walisahau Mungu. Walisahau vile Mungu alikuwa amewaokoa kutoka Misri na kuwaongoza salama mpaka kwa nchi yao. Waisraeli walianza kuabudu sanamu zilizotengenezwa kwa miti na mawe. Hawakuomba Mungu kumuuliza awalinde.

Wakanaani walikuwa adui wa Waisraeli. Bunde tu Wakanaani walianza kushambulia Waisraeli. Walifukuza Waisraeli kutoka kwa boma zao. Waliiba mavuno yao. Waliwashambulia hata kwa barabara. Wakanaani waliteza Waisraeli kwa miaka ishirini.

Nahodha wa jeshi la Wakanaani aliitwa Sisera. Sisera alikuwa na magari ya chuma mia tisa na jeshi la nguvu sana. Waisraeli walikuwa na jeshi ndogo sana. Hawakuwa na magari. Walikuwa na silaha chache.

Wakanaani waliendelea kuwa na nguvu. Walifanya Waisraeli wakaumia sana. Mwishowe Waisraeli walikumbuka kwamba Mungu alikuwa amewasaidia sana, hata akawapa nchi ya kuiishi. Waisraeli waliacha kuabudu sanamu ya miti na mawe. Waliomba Mungu. Waliuliza Mungu awasamehe kwa kuwa waovu sana. Waliuliza Mungu awaokoa kutoka kwa Sisera na Wakanaani.

Mungu alifurahi sana kwa sababu Waisraeli walimrudia. Aliwasamehe maovu yao. Mungu alichagua Baraka kuongoza jeshi la Israeli kupigana na Sisera na Wakanaani. Baraka alienda kuona Debora. Debora alikuwa nabii. Aliishi kwa Mlima wa Efraimu ndani ya hema chini ya mti wa mnazi. Debora aliambia Baraka chenye Mungu alitaka afanye. Debora aliambia Baraka achukue wanajeshi elfu kumi. Halafu aende kwa Mlima wa Tabori. Kule Mungu atamsaidia ashinde Sisera na Wakanaani.



Baraka aliogopa Sisera na magari yake mia tisa ya chuma. Hakuamini Mungu kamili. Baraka aliambia Debora, "Nitaenda ikiwa utaenda na mimi."

Debora alikuwa na imani kwa Mungu. Alikubali kuenda kusaidia Baraka. Lakini Debora aliambia Baraka, "Wewe haukuamini Mungu kabisa, kwa hivyo utukufu wa kushindi Sisera hautakuwa wako. Mwanamke atauwa Sisera na atapata utukufu."

Debora na Baraka walienda na jeshi la watu elfu kumi kwa Mlima wa Tabori. Sisera alikuja kupigana nao. Sisera alikuwa na magari ya chuma mia tisa na jeshi kubwa mno. Baraka na jeshi lake ndogo aliangalia jeshi kubwa la Sisera likija n'gambo yao. Jeshi la Baraka lilikuwa ndogo sana – lakini Mungu alikuwa akiwapigania.

Debora aliambia Baraka, "Leo Mungu atakusaidia ushinde Sisera na jeshi lake lote. Bwana ameenda mbele yako kwa vita. Enda upesi."

Baraka na Jeshi lake walitoka kwa Mlima wa Tabori. Waliteremka kwa bonde kuelekea kwa Sisera na Wakanaani. Mungu alileta dhoruba kubwa. Maji mingi ya mvua ilienda kwa bonde. Kijito cha bonde kiliendelea na kikawa mto mkubwa mpaka bonde yote ikajaa maji. Farasi na magari ya Sisera ilifanya matope mingi nzito. Kwato za farasi zilikwama kwa matope na magurudumu ya magari nayo yalikwama kabisa. Jeshi la Sisera halingesonga. Farasi na magari yote ilikwama kwa matope. Kulikuwa na mahangaiko. Jeshi la Sisera walipinduka na kutoroka. Walitoroka wakifuata kando ya bonde. Waisraeli waliwafuata na wakaua wengi yao.

Sisera aliaacha gari lake na kutoroka. Alijaribu kutoroka kutoka kwa Baraka na Waisraeli. Sisera alikimbia kwa muda mrefu. Alikuwa na kiu na kuchoka pia. Mwishowe alifika kwa hema ya Yaeli. Yaeli alikuwa mtu wa kabila ya Mkeni. Wakeni walikuwa marafiki na Wakanaani. Sisera alifikiri kwamba ataokoka akienda kwa hema ya Yaeli.

Yaeli alikuwa na imani kwa Mungu. Alijua kwamba Sisera ni adui mkubwa wa watu wa Mungu. Yaeli alienda nje ya hema yake. Alijifanya kumkaribisha Sisera. Alimwambia, "Kuja upumzike kwa hema yetu. Usiogope." Yaeli alimtuliza Sisera na akamfunika blanketi. Sisera alikuwa na kiu. Aliomba Yaeli maji ya kunywa. Yaeli alijifanya kwamba Sisera alikuwa mgeni wa heshima. Alimpa maziwa badala ya maji. Alimletea maziwa akunywe na chakula kizuri sana.

Sisera alifikiri alikuwa salama na Yaeli. Aliuliza Yaeli asimame mlangoni akichunga wakati yeye analala. Bunde tu Sisera alilala fofofo. Yaeli alichukua moja ya misumari ya kushika hema. Akachukua nyundo. Yaeli alienda pole pole kwa Sisera alipokuwa akilala. Aligonga msumari kwa kichwa cha Sisera. Sisera akafa.

Bunde tu Baraka akafika. Alikuwa anajaribu kumshika Sisera. Yaeli alimwonyesha Sisera amekufa. Mungu alisaidia Baraka kushinda Wakanaani. Lakini Sisera aliuwawa na mwanamke kama vile Debora alitabiri. Mungu alisaidia Waisraeli kushinda adui wao. Waisraeli waliabudu Mungu tena. Walikuwa na amani kwa miaka arobaini.